MSURURU WA KUBADILISHA, KUGEUZA NA KUZUSHA

# WASIA WA MTUME MTUKUFU WA DARAJA ﷺ KATIKA VITA



SW

SANAD

TOLEO LA NNE 4

*Kwa Jina La (Mwenyezi Mungu) Mrehemevu Mno Wa Mwingi Wa Rehma.*

# *KUTAHADHARISHA KUTOKAMANA NA KUUWA PASI NA NJIA YA HAKI*


Kutoka kwa ibn Abbas kuwa mtu alimjilia yeye akasema, “Waonaje mtu aliyemuua mtu kimakusudi?” Akasema kumjibu kwa mujibu wa Qurani, “{Malipo yake Jahannam (moto) milele ndani yake na amemlaani na amemuandalia yeye adhabu kubwa}. Hakika imeteremshwa katika mwisho ambao kwamba iliteremshwa. Haikufutwa na chochote mpaka akafa Mtume ﷺ na wala haikushuka wahyi [ufunuo] baada ya Mtume ﷺ.” Huyu mtu akasema, “Waonaje akitubu na akaamini na akatenda mema kisha akaongoka?” Ibn Abbas akasema, “Vipi atatubu na hakika nilimskia mtume ﷺ akisema, “Ameangamia mtu aliyemuuwa mtu kimakusudi. Ataletwa siku ya kiama ilihali aliyemuua ameshika kwa mkono wake wa kushoto au kulia au hali ya kumshika kichwa chake kwa mkono wa kulia au kushoto huku zikitiririka damu mishipa yake mpaka mbele ya arshi atasema, ‘Eeh Mola muulize mja wako kwa lipi aliloniuwa?"(1).

# KULAZIMIANA NA AHADI PAMOJA NA MUUWAJI MPIGANAJI

Hakika limefika umuhimu wa jambo hili kwa Mtume ﷺ kuwa amejiweka mbali kutokamana na mwenye kufanya vitimbi hata kama ni Muislamu na hata kama mwenye kufanyiwa kitimbi ni kafiri yeyote. Amesema Mtume ﷺ “Yeyote mwenye kumwaminishia mtu damu yake kisha akamuuwa yule mtu basi mimi nipo mbali kutokamana na mauwaji na hata muuliwa ikiwa ni kafiri.” 2

EHH MOLA MUULIZE
MJA WAKO ALINIUWA
KWA LIPI

?



1- Isnadi yake ni sahih ameitoa Imam Ahmad katika musnad yake.

2- Bukhari katika at-Tarikh al-Kabir 3/322 na temshi ni lake, Ibn Hibban (5982) na al-Bazzar (28).




# MUSIEUWE MTOTO WALA MWANAMKE WALA MZEE MKONGWE

## KUHIFADHI MAISHA YA ADUI

Amesema Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akitoa wasia kwa jeshi katika vita vya Mu`tah, “Nawahusieni kwa kumuugopa Mwenyezi Mungu na kwa pamoja na walioko na nyinyi, kutokamana na Waisilamu musimuue mtoto wala musimuuwe mwanamke wala mzee mkubwa mkongwe.”(3).

3- Ameipokea hadithi hiyo Muslim.Diriwayatkan oleh Imam Muslim.




# MUSIMUUE ALIYE-JITENGA KWA IBADA WALA HAWAVUNJIWI MAKANISA YAO

## KATIKA KUCHUNGA UHURU WA DINI YA ADUI

Amesema Mtume ﷺ, “Wala musimuue aliyejitenga kwa ajili ya ibada katika utawa,”[4] “Musimuuwe Padri,[5]“Hawavunjiwi makanisa yao.”[6]

( 4) Ameipokea hadithi hiyo Muslim.
(5) Amepokea al-Bayhaqi katika as-Sunan.
(6) Mtume alisuiuhiana na watu wa Najran wasivunjiwe makanisa yao. Mapokezi Abu Dawud katika Sunan.



# MUSIVUNJE MAJENGO

## KUJENGA NA KUIMARISHA SIO KUHARIBU NA KUVUNJA

Amesema Mtume ﷺ, “Musiukaribie mtende wala msiukate mti na wala msivunje jengo.”
Na amesema ﷺ “Wala msichinje ngamia wala ngombe ila kwa ajili ya kula. Msimgharakishe nyuki wala msiwachome”[7].

7- Amepokea al-Bayhaqi katika as-Sunan al-Kubra.

# UPOLE NA HURUMA KWA WANYAMA

Alipoenda Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutoka al-Arj kukawa kati ya al-Arj[8] na Talob[9] na zote zikiwa ni sehemu, alimuona mbwa akitoa sauti kwa sababu ya watoto wake na wao wakiwa pembezoni mwake wakimyonya. Akaamrisha mtu katika masawahaba zake aitwae Ju'ayl bin Suraqa asimame upande wa mbwa ili jeshi lisimuudhi mbwa wala watoto wake.[10]

8- Al-Arj ni sehemu kati ya Makka na Madina.
9- Talob ni maji katika njia iliyoko kati ya Madina na Makka.
10- Al-Maghazi ya al-Waqidi (ukurasa 804)



## KUKATAZA KUADHIBU KWA KUKATA VIUNGO

Kutoka kwa Imran bin Husayn amesema, “Hakusimama Mtume ﷺ kutukhutubia ila ametuamrisha sisi kwa sadaka na ametukataza sisi na kukata viungo.” (11).

## KUWATENDEA WEMA MATEKA WA KIVITA

Asema Mwenyezi Mungu: {Na huwalisha chakula juu ya kupenda kwake maskini na yatima na wafungwa matekwa.}[12]
Na amesema Mtume ﷺ, “Nawausieni kheri kwa mateka.” [13].

11-Ameipokea Ahmad na Abu Dawud.
12- Quran (Insan:8)
13- Kutoka hadithi ameitoa at-Tabarani kwa isnadi iliyo nzuri.

# NAWAUSIENI KHERI KWA MATEKA



## KUSAMEHE NA KULIACHIA MBALI NA KUTOPENDA KULIPIZA KISASI

Kisha hakika Mtume ﷺ hakuwa akisamehe watu ambao hawajipeleki haraka au kujichelewasha sana katika msururu wa matukio tu bali alikuwa akisamehe mapote kamili. Miongoni mwa sehemu za Mtume ﷺ neno lake katika ufunguzi wa Makka kwa waliompiga vita miaka ishirini:
"Enyi kongamano la Maqurayshi, nini mwaona kuwa mimi ni mwenye kuwafanyia nyinyi?"
Wakasema: "Kheri, ndugu mkarimu na mtoto wa ndugu mkarimu." Akasema, "Nendeni basi nyinyi mko huru." [14]

NENDENI
BASI NYINYI MKO HURU...



14- Ibn Hisham: as-Sira an-Nabawiyya 2/411, na Ibn Hajar: Fath al-Bari 8/18.

# UFUPILIZO

Katika yaliyotangulia, tumeona wasia wa Mtume (Rehema na Amani zimshukie na jamaa zake) ambao sisi twahitaji zaidi katika amani kabla ya kwenye vita, imebainika hali hii tunyaoiona sasa ya wanaodai wanafanya wanayoyafanya ya israfu katika kuuwa na kuwafanyia uadui watoto na wanawake na kuvunja kila lenye kuimarisha maisha kwa kuchoma na kubomoa nchi na miji, na wanadai kuwa wanayafanya hayo kulingana na uislamu. Ambapo kwamba kusema hivi ni upotoshaji wa wazi wa yale aliyoyasema Mtume ﷺ kutokamana na miongozo na wasia kwa majeshi wakati akisema hali ya kuwapa wasia jeshi la Mu`tah: "Nawahusieni na walionanyi kutokamana na waisilamu kheri. Piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa aliyemkufuru Mwenyezi Mungu. Msifanye vitimbi wala msifanye khiana na wala msimuue mtoto wala mwanamke wala mzee mkongwe wala aliyejitenga kwa ajili ya ibada katika utawa wake. Wala musiukate mtende wala musikate miti wala musivunje majengo.[15]

Na amesema Mtume Muhammad (Rehema na Amani zimshukie na jamaa zake na maswahaba zake), "Musiuwe mtoto wala mwanamke wala mzee mkongwe wala mgonjwa wala wamonaki wala musikate miti yenye kutoa matunda wala musiharibu majengo wala musichinje ngamia wala ngo'mbe illa kwa ajili ya kula wala msiwaangamzie nyuki wala musiwateketeze.[16]



**Musiuwe mtoto wala mwanamke wala mzee mkongwe wala mgonjwa.**
**Wala musimuue mtu aliyejitenga kwa ajili ya ibada na wala musimvunjie sehemu yake wala wamonaki wala msivunje majengo.**
**Wala msikaribie mtende wala msikate mti wenye kutoa matunda.**
**Wala msivunje majengo wala msiharibu palipo imarika.**
**Msichinje ngamia wala ngo'mbe ila kwa ajili ya kula.**
**Wala msiangamize nyuki wala musiwateketeze.**
**Msifanye vitimbi, wala msikate viungo wala msifanye khiana.**

**Nawausieni kheri kwa mateka.**

(15) As-Sunan al-Kubra ya al-Bayhaqi juzuu ya tisa ukurasa 69, na Subul al-Huda wa ar-Rashad j juzuu ya 6 ukurasa 146.
(16) Amepokea al-Bayhaqi katika as-Sunan.

# MSURURU WA KUBADILISHA NA KUPOTOSHA NA KUZUSHA

Amesema Mtume (Rehema na Amani zimshukie na jamaa zake), " Wataibeba hii elimu kwa kila watu waadalifu wake na watauweka mbali upotevu wenye kuvuka mipaka na uzushi wa watu wenye kuleta batili na bayana za wajinga." [17]

Wamefahamu baadhi ya watu wenye fikra potevu na fahamu mbaya maneno ya Mwenyezi Mungu na maneno ya Mtume Wake ﷺ kwa namna isiyo ambatana na mfumo wa kielemu iliyoridhiwa kutoka kwa salaf (wema waliotangulia) wala haziambatani na makusudio na misingi mikubwa ya wahyi (ufunuo) wa kimola.

Walikusudia baadhi za aya za Quran Tukufu ambazo zilishuka juu ya wasiokuwa waisilamu wakazishukisha kwa waisilamu na wakachukuwa aya zilizokuja kwa njia ya kuvuwa wakazifanya miongini mwazo hukumu yenze kuenea wakageuza na kupendua maana ya meneno ya Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume Wake Mtukufu kwa namna iliyopelekwa katika kuthibitisha au kuuandika fahamu iliyomakosa vibaya katika akili ya baadhi ya waisilamu walio wajinga iliyofanya kutoa ntija ya tabia na vitendo visivyokuwa na mafungamani na dini ya Kiislamu isiyokuwa na urongo.

Tunaweza kutambua katika madhumuni ya msururu juu ya ambao kwamba walitoka ndani yake watu wenye hizi fikra za makosa kutokamana na kubadilisha au kupotosha kwa maana ya maneno ya Mwenyezi Mungi na maneno ya Mtume Wake na kwa fahamu wa watu wema waliotangulia.

17- Hadithi tangufu ameisahihisha Ibn Abdul Bar. Imeipokea kutoka kwa Ahmad Bin Hanbal kuwa yeye amesema, "Ni hadithi sahihi."



DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION
SANAD
www.sanad.network
twitter: @sanadnetwork
facebook.com/sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork